

IDARA YA AFYA YA NEW MEXICO
RIDHAA YA MZAZI/MLEZI WA MTOTO MDOGO ANAYEPOKEA CHANJO YA COVID-19

Mimi, _____, nikiwa mzazi, mlezi au mwakilishi halali aliyeidhinishwa kutoa ridhaa ya matibabu kwa mtoto aliyeorodheshwa hapa chini, ninatoa ridhaa na kibali kwa watoa huduma wa matibabu walioidhinishwa wa Idara ya Afya ya New Mexico (New Mexico Department of Health, NMDOH) kutoa chanjo ya COVID-19 kwa mtoto wangu iwe nipo au niwe sipo mwenyewe.

Ninaelewa kwamba kufuatia kutolewa kwa chanjo, NMDOH itamfuatilia mtoto wangu.

- Ikiwa mtoto wangu hajazindikishwa na mtu mzima, mtoto wangu atafuatiwa kwa kipindi cha dakika 30 kwa athari yoyote mbaya.
- Ikiwa mtoto wangu amezindilishwa na mtu mzima, mtoto wangu anaweza kuruhusiwa kuangaliwa na mtu mzima baada ya kipindi cha dakika 15 kwa athari yoyote mbaya.
- Ikiwa mtoto wangu ana hali ya kimatibabu inayoongezea hatari yake ya athari, mtoto wangu atafuatiwa kwa kipindi cha dakika 30 kwa athari yoyote mbaya.

Iwapo athari itatokea, ninaidhinisha matibabu yoyote yanayofaa ya dharura na ninaelewa kwamba NMDOH itaniarifu haraka iwezekanavyo. Ninafahamu zaidi kwamba ridhaa hii inaweza kuthibitishwa aidha ana kwa ana au kwa maneno kwa simu kabla ya chanjo kutolewa ikiwa kuna maswali.

Ninaelewa kwamba mtoto wangu atapokea chanjo ya COVID-19 iliyoidhinishwa na Shirika la Usimamizi wa Chakula na Dawa, chini ya Idhini ya Matumizi ya Dharura.

Nimepewa "MAELEZO YA WAPOKEAJI NA WATOA HUDUMA" ya chanjo ya COVID-19.

[Maelezo ya EUA ya Chanjo ya Pfizer-BioNTech ya COVID-19 kwa Wapokeaji na Watoa Huduma \(fda.gov\)](https://www.fda.gov)

[Maelezo ya Wapokeaji wa Chanjo | EUA | Chanjo ya Moderna ya COVID-19 \(modernatx.com\)](https://www.modernatx.com)

[Maelezo ya EUA ya Chanjo ya Janssen ya COVID-19 kwa Wapokeaji na Watoa huduma \(janssenlabels.com\)](https://www.janssenlabels.com)

Ninaelewa faida na hatari za chanjo na ninatoa ruhusa kwa mtoto wangu kuchanjwa.

Chanjo Inayotolewa **Pfizer-BioNTech**

Jina la mtoto anayepokea chanjo: _____

Nambari ya Thibitisho ya mtoto: _____

Jina la mzazi au mlezi halali: _____

Saini ya mzazi au mlezi halali: _____

Tarehe: _____

Nambari ya simu ya nyumbani ya mzazi au mlezi halali: _____

Kwa Wafanyakazi PEKEE: Chaguo la kumfanya mtoto kupata chanjo zinajumuisha:

1. Mzazi kuhudhuria tukio na kutia saini fomu ya ridhaa iliyoidhinishwa kituoni
2. Mtoto kuleta fomu iliyotiwa saini kwa tukio bila mzazi kuwepo